Ombi la Kurekebisha Bei za Majisafi na Majitaka la

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SINGIDA (SUWASA)

Utangulizi

1. Tarehe 21 Juni, 2011, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ("EWURA") ilipokea ombi kutoka SUWASA kuhusu yafuatayo:

(a) kuongeza bei ya maji kwa wateja wa majumbani wenye mita kwa kiwango cha asilimia 8 hadi 15, kutoka TZS 480 hadi TZS 550 kwa mita ya ujazo kwa matumizi chini ya mita 10 za ujazo; na kutoka TZS 600 hadi TZS 650 kwa mita ya ujazo kwa matumizi zaidi ya mita 10 za ujazo;

(b) kuongeza bei ya maji kwa wateja wa taasisi wenye mita kwa kiwango cha asilimia 5 hadi 6, kutoka TZS 660 hadi TZS 700 kwa mita ya ujazo kwa matumizi chini ya mita 10 za ujazo; na kutoka TZS 715 hadi TZS 750 kwa mita ya ujazo kwa matumizi zaidi ya mita 10 za ujazo;

(c) kuongeza bei ya maji kwa wateja wa taasisi za kidini wenye mita kwa kiwango cha asilimia 8, kutoka TZS 600 hadi TZS 650 kwa mita ya ujazo kwa matumizi chini ya mita 10 za ujazo; na kutoka TZS 650 hadi TZS 700 kwa mita ya ujazo kwa matumizi zaidi ya mita 10 za ujazo;

(d) kuongeza bei ya maji kwenye magati (kiosks) kwa asilimia 100 kutoka TZS 500 hadi TZS 1,000 kwa mita ya ujazo;

(e) kuongeza bei ya kuunganisha maji kwa wateja wapya kwa kiwango cha asilimia 25 hadi 60, kutoka TZS 40,000 hadi TZS 50,000 kwa wateja wapya wa majumbani; na kutoka TZS 50,000 hadi TZS 80,000 kwa wateja wapya wa biashara na taasisi; na

(f) kuongeza tozo la ukodishaji wa mita kwa kiwango cha asilimia 150 hadi 300; kutoka TZS 500 hadi TZS 2,000 kwa mwezi kwa wateja wa majumbani; na kutoka TZS 2,000 hadi TZS 5,000 kwa mwezi kwa wateja wa biashara na taasisi.

Ushirikishwaji

2. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(h) cha Sheria ya Mamlaka ya

wa Wadau

Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, EWURA ilifanya taftishi kuhusu uhalali wa ombi la kurekebisha bei za huduma ya maji za SUWASA. Taftishi hiyo ilihusisha tathmini ya masuala ya kiuchumi na ya kiufundi pamoja na kufanya mkutano wa taftishi tarehe 9 Novemba 2011 katika mji wa Singida ili kusikia maoni ya wadau.

3. Wakati wa mkutano wa taftishi, SUWASA iliwasilisha mada juu ya ombi lake ikielezea sababu na uhalali wa mapendekezo ya nyongeza ya bei na gharama. Wadau wotewakiwemo wateja wa SUWASA, Baraza la Ushauri la Serikali (*Government Consultative Council* ("GCC")), na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (*Consumers Consultative Council* ("CCC")) walipata fursa ya kuchunguza na kutoa maoni yao kuhusiana na uhalali wa ombi hilo. SUWASA vile vile ilipewa fursa ya kujibu hoja za wadau kwenye mikutano hiyo na kuwasilisha EWURA majibu ya hoja za wadau kwa maandishi.

4. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji lilihoji, pamoja na mambo mengine, kutokupandishwa kwa bei za wateja wa biashara, wateja wasio na mita kulipa kiasi sawia bila kujali siku wanazopata maji, kiwango cha juu cha maji yanayopotea, na idadi kubwa ya wateja waliokatiwa maji.

5. GCC walihoji, pamoja na mambo mengine, muda mfupi ambapo bei zilizopo zimetumika toka zilipoidhinishwa, gharama kubwa za utawala, idadi kubwa ya wateja waliokatiwa maji, takwimu ya idadi ya watu iliyotumika na hitaji la SUWASA kutafuta vyanzo mbadala vya maji.

6. Kutoka kwa wateja wa SUWASA, kulikuwa na malalamiko juu ya bili za maji zisizoendana na matumizi halisi zinazosababisha na mita kusoma kiwango kilichokosewa, mgawanyo wa maji usio sawia, bei kubwa zinazotozwa na wauza maji binafsi, na kushindwa kwa SUWASA kuweka mikakati ya kupeleka maji maeneo ambayo bado hayajafikiwa.

7. Wakati wa kuhitimisha taftishi tarehe 23 Novemba 2011, SUWASA iliweza kujibu hoja za wadau kwa kiasi cha kuridhisha; na EWURA ilikusanya taarifa za kutosheleza kufanya maamuzi. Wakati wa uchambuzi wa ombi, SUWASA ilitakiwa, na ilitoa maelezo ya ziada kuhusu ombi hilo

Uchambuzi na marekebisho

8. Kufuatia kukamilika kwa taftishi hiyo, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la nyongeza ya bei lina mantiki na ni halali, isipokuwa gharama kubwa za uendeshaji na matengenezo ambazo zimerekebishwa kutoka TZS 1,085 Milioni hadi TZS 962 Milioni baada ya uchunguzi wa kina wa gharama na shughuli zinazotegemewa kufanyika.

9. Maombi na marekebisho ya mahitaji ya mapato ya SUWASA ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali hapa chini

Maamuzi

Jedwali 1: Mahitaji ya Mapato

	Mapendekezo ya Mapato, 2011/12	**Mapato Yaliyoidhinishwa, 2011/12**
GHARAMA ZA UENDESHAJI NA MATENGENEZO	**TZS**	**TZS**
Uzalishaji Maji	176,558,900	176,558,900
Usambazaji	29,950,000	29,950,000
Marekebisho na Matengenezo	68,450,000	68,450,000
Utawala	180,520,400	183,870,400
Uzalishaji Maji	577,151,916	450,559,856
Usambazaji	29,035,000	29,035,000
Marekebisho na Matengenezo	9,700,000	9,700,000
Utawala	9,150,000	9,150,000
Uzalishaji Maji	5,000,000	5,000,000
Jumla Ndogo	**1,085,516,216**	**962,274,156**
Uchakavu	-	-
Miradi kutumia fedha za ndani	45,000,000	45,000,000
JUMLA MAHITAJI YA FEDHA	**1,130,516,216**	**1,007,274,156**

10. Katika kikao chake cha tarehe 16 Desemba 2011, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ilijadili ombi la SUWASA na kutoa maamuzi kama inavyoonyeshwa kwenye Agizo hapa chini:

SHERIA YA MAJISAFI NA MAJITAKA

(SURA NA 272)

AGIZO Na. 11-020

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d) cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, 2009)

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA SINGIDA ("SUWASA"), AGIZO LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI, 2011

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida ("SUWASA"), Agizo la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji, 2011.

Marekebisho ya Bei

2. Bei za maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Singida ("SUWASA") zinarekebishwa kulingana na Majedwali yaliyopo katika Agizo hili.

3. Bei zilizopitishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 30 Juni 2013 aub kabla ya hapo, SUWASA inatakiwa:

(i) kupunguza kiwango cha maji yanayopotea kutoka kiwango cha sasa cha 25% hadi 20% or chini ya hapo;

(ii) kuongeza kiasi cha wateja wenye mita za maji kutoka kiwango cha sasa cha 69% hadi 100%; na

(iii) Kuboresha progamu ya kuandaa bili ili iweze kutambua malipo yanayofanyika baada ya kutoa ripoti ya mwezi ifikapo tarehe 30 Juni 2012;

Masharti

(b) ifikapo au kabla ya tarehe 30 Juni 2012, SUWASA, kwa kufuata mwongozo uliotolewa na EWURA, itawasilisha EWURA marejeo ya Mpango wake wa Biashara (Business Plan), Mpango wa Fedha wa muda mrefu (Longterm Financial Plan) na Mpango wa Usimamizi wa Mali na Rasilimali (Asset Management Plan);

(c) SUWASA itawasilisha pamoja na ripoti zake nyingine, ripoti juu ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

(i) ukarabati wa pampu za maji zilizoharibika na ufungaji wa pampu mpya kwenye visima vya Uhasibu na Kititimo;

(ii) ujenzi wa bomba kuu la maji linalounganisha visima vya Utemini na Kititimo na vituo vya kusukumia maji (booster stations);

(iii) Ujenzi wa fensi kuzunguza maeneo ya visima vya maji; na

(iv) Ujenzi wa jengo jingine la ofisi;

(d) ifikapo tarehe 30 Septemba 2012 au kabla, SUWASA itawasilisha ushahidi kwamba imetengeneza na kutekeleza mpango wa kuwafikia wateja wake. Ripoti ya utekelezaji wa mpango huo itawasilishwa pamoja na ripotiza SUWASA zitakazowasilishwa EWURA na ripoti hiyo itatumiwa na EWURA katika kutathmini ombi lingine lolote la mabadiliko ya bei; na

(e) SUWASA itaendelea kuwasilisha kwa EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa muibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa SUWASA ikilinganiswa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Majitaka nchini. EWURA itazingaitia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na SUWASA katika siku zijazo.

Utenguzi

4. Agizo Na. 10-018 la tarehe 1 Desemba, 2010 la Marekebisho ya Bei za Maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Singida linatenguliwa.

KIAMBATANISHO

Jedwali 1: Bei za Wateja Wenye Dira za Maji

Kundi	**Matumizi ya Maji**	**Bei ya Sasa**	**Bei Iliyoidhinishwa**
	(m^3)	**(TZS/m^3)**	**(TZS/m^3)**
Majumbani	0-10	480	550
	>10	600	650
Taasisi	0-10	660	700
	>10	715	750
Biashara	0-10	650	650
	>10	700	700
Taasisi za Kidini	0-10	600	650
	>10	650	700
Magari ya Maji (Bowsers)	-	1,500	1,500
Magati (Kiosks)	TZS 20/20 lita	500	TZS 20/20 lita

Jedwali 2: Bei kwa Wateja Wasio na Dira za Maji

Kundi	**Bei ya sasa**	**Bei Iliyoidhinishwa**
	TZS/Mwezi	**TZS/Mwezi**
Majumbani	8,000	8,000
Biashara	15,000	15,000
Taasisi	15,000	15,000
Taasisi za dini	12,000	12,000

Jedwali 3: Tozo na Ada Mbalimbali

Aina ya Tozo/Ada	**Kundi la Wateja**	**Bei ya Sasa**	**Bei Iliyoidhinishwa**
		TZS/Mteja	**TZS/Mteja**
Ada ya Maunganisho Mapya	Majumbani	40,000	50,000
	Biashara	50,000	80,000
	Taasisi	50,000	80,000
Tozo ya dira	Majumbani	500	1,000
	Biashara	2,000	2,500
	Taasisi	2,000	2,500
Ada ya Kurejesha Huduma	WOTE	10,000	10,000
Ada ya kubadilisha maungio ya maji	WOTE	10,000	10,000

Dar es Salaam HARUNA MASEBU

Mkurugenzi Mkuu

16 Desemba 2011